# TAARIFA KWA UMMA

OFISI YA WAZIRI MKUU KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU IMEANZISHA MPANGO WA KUSIKILIZA NA KUSHUGHULIKIA MALALAMIKO YANAYOTOKANA NA MASUALA YA KAZI.

TAASISI ZITAKAZOHUSIKA NI IDARA YA KAZI, MIFUKO YA HIFADHI YA JAMII (NSSF NA PSSSF) MFUKO WA FIDIA KWA WAFANYAKAZI (WCF), MAMLAKA YA AFYA NA USALAMA MAHALA PA KAZI (OSHA) PAMOJA NA VYAMA VYOTE VYA WAFANYAKAZI NA WAAJIRI.

KWAHIYO, WAFANYAKAZI, WAAJIRI NA WADAU WOTE WENYE MALALAMIKO KUHUSIANA NA KAZI MNATANGAZIWA KUWAPO KWA KILINIKI YA MALALAMIKO YA KAZI KILA SIKU ZA IJUMAA YA MWISHO WA MWEZI.

KWA MWEZI MACHI 2024 KILINIKI ITAFANYIKA IJUMAA YA TAREHE 29 (29/03/2024) KUANZIA SAA 4 ASUBUHI HADI SAA 9 ALASIRI KATIKA UKUMBI WA JENGO LA OFISI YA WAZIRI MKUU.

JENGO LIPO BARABARA YA STESHENI, JENGO NAMBA 8, MKABALA NA KITUO CHA MAFUTA CHA TOTAL, PEMBENI YA HOSPITALI YA CF.

TAFADHALI USOMAPO TAARIFA HII MWARIFU NA MWINGINE.

**IMETOLEWA NA OFISI YA IDARA YA KAZI, MKOA WA MWANZA**

**26/02/ 2024**